# TAWHIYD NA NIDHAMU YA DUNIA

<"xml encoding="UTF-8?>

BISMILAHI RAHMANI RAHIYMI

KWA JINA LA MWENYEEZI MUNGU MWINGI WA REHEMA MWENYE KUREHEMU

TAWHIYD NA NIDHAMU YA DUNIA

Hakuna shaka ya kuwa Mwenyeenzi Mungu Mtukufu ameviumba vitu vyote duniani vikiwa -:katika nidhamu maalum, na Allah (s.w) anasema

الَّذِى خَلَقَ سَبْعَ سَمَاوَاتٍ طِبَاقاً مَّا تَرَي فِى خَلْقِ الرَّحْمَنِ مِن تَفَاوُتٍ فَارْجِعِ الْبَصَرَ هَلْ تَرَي مِن فُطُورٍ[1]

Aliye umba mbingu saba kwa matabaka. Huoni tafauti yoyote katika uumbaji wa Mwingi wa ?Rehema. Hebu rudisha nadhari! Unaona kosa lolote

Nidhamu hiyo ya uumbaji inathibitisha kuwepo kwa Mola mmoja, na Mola huyo ndiye .aliyeviumba vitu vyote duniani, na kasha akaviweka katika nidhamu maalumu

Kwani kama kuna mungu zaidi ya mmoja kusingelikuwa na nidhamu yoyote na kungelikuwa na hitilafu na tofauti baina ya muumba mmoja na mwengine, basi natuzingatie ayah ii .inayothibitisha kauli hiyo

لَوْ كَانَ فِيهِمَا آلِهَةٌ إِلاَّ اللهُ لَفَسَدَتَا فَسُبْحَانَ اللهِ رَبِّ الْعَرْشِ عَمَّا يَصِفُونَ[2]

Lau wangeli kuwamo humo miungu wengine isipo kuwa Mwenyezi Mungu basi bila ya shaka hizo mbingu na ardhi zingeli fisidika. Subahana 'Llah Ametakasika Mwenyezi Mungu,Bwana wa .A'rshi (Kiti cha Enzi), na hayo wanayo yazua

Maelezo kuhusiana na aya

Hii ni kawaida isiyoanguka kuwa “ Mafahali wawili hawakai zizi Moja” Basi wangekuwako waungu wawili wangepigana daima hata mmoja amshinde mwenziwe au wauwane; udhia .wishe

Na muda wote huo- wa kuzatiti vita mpaka kutiana mikononi- hawatashughulikia jengine ila ?hilo tu la kutafuta kushinda. Tena mambo atayaendesha nani

Na wakiwa wengi zaidi kuliko wawili ndiyo vivyo hivyo- watapigana mpaka wamalizane. Au-tuseme wapatane. Na wakipatana basi watauparaganya tu mwenesho wa ufalme wao kwani ”.kwa “Manahodha Wengi jahazi huzama

.Basi Mwenyeenzi mungu ni mmoja tu. Wahadahu Laa Sharyka Lahuu

Na watu mambo yao ndiyo vivi hivi. Yakiwa yanaendeshwa na chungu ya wakubwa – na kila .mmoja hakubali kumsikiliza mwenziwe – basi yataharibika tu

Ndiyo maana Mtume akihimiza kuwa sharti – katika kila mkusanyiko – apatikane mkubwa anayetiiwa na wote kwa anayoyasema yakaingia shariani;au akilini yakiwa hayahusu sheria. Akisema Mtume kuwa watu – wakishakuwa watatu – katika msafara wao – basi sharti wamfanye mmoja mkubwa wao kwani mambo hayatengenei yakiwa fujo, ovyo ovyo, hayana mkubwa. Inasemwa kwa kiarabu; Laa yasluhunaasu fawdhaa Laa saraatalahum. Yaani mambo .hayatengenei yakiwa ovyo,hayana mkubwa au wakubwa wa kuyaendesha

Na sharti ya hao wakubwa – ilivyoweka uislamu – ni wawe na elimu nzuri na utambuzi kamili. . Ikiwa si hivyo, si wakubwa hao, wala mambo hayataendelea

.Inasemwa: Walaa saraata Idhaa Fuhhaaluhum saaduu

TAWHIYD ( KUAMINI MOLA MMOJA) NDANI YA SHERIA ZA VITABU VYA MWENYEENZI MUNGU

Vitabu vyote alivyoviteremsha Mwenyeenzi Mungu (s.w) vinathibitisha sheria moja , Nayo ni .kuwa na imani ya Mola mmoja tu

Ijapokuwa “ tawhiyd” na kuamini Mola mmoja ni dalili moja wapo inayoonesha nidhamu ya dunia, lakini vile vile sheria ya vitabu vyote vya Mwenyeenzi Mungu yaani (Qur-ani, Tawrati, na Injili) vimekuja na sheria moja tu, nayo ni kuamini Mola mmoja. Imamu Ali (a.s) katika wasia -:wake aliomuusia mwanawe Imam Hassan (a.s) anasema

[3]“واعلم يا بنى انه لو كان لربک شريک لاتتک رسله و لرايت اثار ملکه و سلطانه”

Ewe mwanangu elewa kuwa kama Mwenyeenzi Mungu angelikuwa na mshirika, Mitume yake .(ingelikuja kwako wewe, na ungeliona alama na uwezo wake Allah (s.w

Ijapokuwa sheria za vitabu vyote vya Mwenyeenzi Mungu zinawiana kifikra na kijamii miongoni

mwa wanaadamu, na zinahitilafiana katika baadhi ya hukumu,ama katika nguzo za dini, akida -:.(itikadi), na tawhiyd hakuna tofauti yoyote . Kama vile anavyosema Allah katika Qur-ani

وَمَا اَرْسَلْنَا مِن قَبْلِكَ مِن رَّسُولٍ إِلاَّ نُوحِى إِلَيْهِ اَنَّهُ لاَ إِلَهَ إِلاَّ اَنَا فَاعْبُدُونِ[4]

Na hatukumtuma kabla yako Mtume yeyote ila tulimfunulia ya kwamba hapana mungu isipo .kuwa Mimi. Basi niabuduni Mimi tu

Surat Mulk aya ya 3 [1]

Surat Anbiyaa aya ya 22 [2]

Nahjulbalagha, barua ya 3 [3]

Surat anbiyaa aya ya 25 [4]

MWISHO